

## ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

Hii inarejelea haki na uhuru ambao wanadamu wote wanastahili. Profa Foundation itaelimisha jamii kuhusu haki za binadamu, ili iweze kusaidia kuzuia matatizo kama vile ukiukwaji wa haki za binadamu mfano kazi za kulazimishwa, ubaguzi wa rangi, ukabila, udini na adhabu za kikatili hivyo jamii itafahamu kuhusu haki za binadamu.



**Anwani itakuwa:**

**KAMATI KUU,  
MTAA WA CHASIMBA, PLOT NO. 54  
MAJIMATITU B' - MBAGALA  
DAR ES SALAAM - TANZANIA**



## KITUO CHA YATIMA

Profa Foundation itaanzisha kituo hicho katika MKOA wa PWANI ambapo kituo hiki kitasaidia watoto yatima, watoto wa mitaani na watoto kutoka makundi maalum kwa kuwapatia makao na mahitaji muhimu kama vile chakula na nguo, hii itaepusha ongezeko la watoto wa mitaani katika jamii zetu.

**PROFA FOUNDATION  
ORPHANAGE CENTRE,  
NYANZA STREET, PLOT NO. 13  
KIGUZA MKURANGA  
PWANI -TANZANIA**


## PROFA FOUNDATION



Ni Taasisi isiyo ya Kiserikali (NGO) ambayo itaendesha shughuli zake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye makao yake makuu mkoani Dar es Salaam. Inakuza Ulinzi wa Jamii katika mkutadha huu wa utaalumu wa kudhibiti hasira, Ulinzi wa Mazingira na kukuza haki za Binadamu .

## ULINZI WA JAMII.

Profa Foundation itajali kuhusu suala la kudhibiti hasira kwa jamii kupitia kuonyesha chanzo chake ambacho kinaweza kuwa dhiki, kutotendewa haki, kufadhaika, kushambuliwa au kutoheshimiwa. Kupitia hilo, jamii itaweza kuondokana na madhara yanayoweza kusababishwa na hasira zinazoweza kuwa kama vurugu, unyanyasaji katika jamii, mapigano ya kimwili na uharibifu wa mali.



Taasisi hii inaweza kuwa kama mlinzi wa jamii kwa kulinda utamaduni wetu kama mitindo ya kuvaa, vyakula ambavyo mbalimbali na sanaa za kazi za mikono Profa Foundation inaweza kusaidia kuzuia uharibifu wa utamaduni wetu, hivyo madhara yanayohusiana na uharibifu wa utamaduni yatatatuliwa. . Umuhimu mwingine wa taasisi hiyo ni kukuza maendeleo ya jamii kwa kushughulikia masuala kama vile umaskini, ukosefu wa usawa, ulemavu wa aina yoyote, Watoto wanaoishi katika mazingira magumu, kuanzisha vituo vya watoto yatima, elimu na huduma za afya kwa kuleta mabadiliko endelevu kwa kusaidia na kuwezesha jamii.

## ULINZI WA MAZINGIRA.

Profa Foundation kama mfano wa asasi zisizo za kiserikali inaweza kuwa na mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira kwa kuunda njia endelevu za uhifadhi wa mazingira ambapo shirika hili litazungumza na watu kwa kuwaelimisha juu ya njia za utunzaji wa mazingira ambazo kwa kuhifadhi mazingira tunaongeza muda au maisha ya aina mbalimbali zinazokaribia kuangamia mfano Faru (Faru).



Hii inaweza kuwa upandaji miti na kuzuia uchafuzi wa mazingira yetu, kujenga uelewa wa jamii ambayo itasaidia kuzuia madhara yanayo husiana na uharibifu wa mazingira ambayo yanaweza kuwa kama ongezeko la joto duniani, uchafuzi wa mazingira na ukame. Mambo yafuatayo ambayo Profa Foundation inaweza kutoa kwa jamii.



Anwani itakuwa:

**KAMATI KUU,  
MTAA WA CHASIMBA, PLOT NO. 54  
MAJIMATITU B' - MBAGALA  
DAR ES SALAAM - TANZANIA**

**Tel: +255 654 795 833  
+255 615 165 833  
+255 762 044 791**

**Email: profafoundation@gmail.com**